# TAASISI YA MWALIMU NYERERE

# NEPAD NA MUSTAKABALI WA UMOJA WA AFRIKA
## MAONI BINAFSI

**YA**

**DR. SALIM AHMED SALIM**

**SEMINA YA WAHESHIMIWA WABUNGE ILIYOANDALIWA NA TAASISI YA BUNGE YA DEMOKRASIA**

*Dar es Salaam,*
*17th December 2002.*

## NEPAD NA MUSTAKABALI WA UMOJA WA AFRIKA

## MAONI YA JUMLA YA DR. SALIM AHMED SALIM

**UTANGULIZI**

Pongezi kubwa wanastahiki kupewa Taasisi ya Bunge na Demokrasia (BFD) ambao kwa ushirikiano na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Taasisi ya Umoja wa Mataifa ya Mpango wa Maendeleo (UNDP) wameandaa Semina hii juu ya Mkakati Mpya wa Ushirikiano baina ya Wadau mbalimbali kwa lengo la kuongeza kasi ya maendeleo ya bara letu. Kwa hakika uamuzi huu unaendeleza desturi na mila za muda mrefu zilizojengeka miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge wa Tanzania wa kujipa fursa ya kutafakari kwa kina masuala mazito yenye maslahi kwa jamii ya Watanzania, bara la Afrika na Dunia kwa jumla nje ya utaratibu rasmi wa Kibunge.

Hata hivyo uamuzi wa kuandaa Semina mahsusi kwa Wabunge ili waitumie fursa hiyo kutafakari kwa kina na kuelimishana au kubadilishana mawazo juu ya maudhui ya mkakati huu mpya wa Ushirikiano baina ya Wadau mbalimbali kwa maendeleo ya bara letu unastahiki pongezi za pekee kwa sababu kuu mbili. Kwanza

Semina hii imeandaliwa katika wakati mwafaka na kwamba inakusudia kuzingatia suala zito linalogusa mstakabali mzima wa taifa letu na bara zima la Afrika. Pili ni kwamba madhumuni ya Semina ni ya tafakuri na ya kimkakati. Waheshimiwa Wabunge wataitumia fursa hiyo si tu kwa kujielimisha na kuelimishana juu ya asma hii kubwa ya bara letu, bali pia kuzingatia taathira za utekelezaji wake katika nyanja na maeneo mbalimbali na vilevile mfungamano wa Mkakati huu na Programu zinazotekelezwa hivi sasa na kila nchi au katika kanda mbali mbali barani Afrika.

**ISIMU NA CHIMBUKO LA NEPAD**

Ili kuelewa vema maudhui na undani wa Mkakati wa NEPAD ni vema kukumbushana chimbuko la Mkakati huo ili nafasi yake iwekwe bayana katika kujadili na kutathmini jitihada za bara letu za kutafuta mikakati endelevu yenye lengo la kulikwamua bara hili kutoka hali ya maendeleo duni na umaskini uliokithiri, jitihada ambayo zilijaribiwa katika mazingira ya karne iliyotangulia.

Hapana shaka sote tunakumbuka kwamba mwaka 1985 wakati Tanzania ikiwa ndiyo Mwenyekiti wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika, Wakuu wa Nchi waliridhia mpango wa kufufua uchumi

katika Bara la Afrika (Africa Priority Programme for Economic Recovery APPER). Hii ilitokana na hali mbaya ya kiuchumi iliyokuwa ikilikabili Bara la Afrika katika kipindi cha muongo wote wa 1980. Mseleleko wa kuzorota kwa uchumi na matatizo mengine ya Kisiasa na Kiuchumi yatokanayo na hali hiyo, ndiyo yaliyopelekea kipindi hicho kuitwa "muongo uliopotea" kw aAfrika. Ndiyo maana katika muongo uliofuata jitihada zaidi zilifanywa kukabili hali hiyo kwa kubaini kiini cha matatizo yanayolikabili bara letu na kubuni mikakati endelevu ya kutuwezesha kukusanya nguvu za pamoja kuamua hatma na mstakabali wa bara la Afrika.

Mkataba wa Abuja wa kuanzishwa kwa Jumiya ya Uchumi ya Bara la Afrka na uamuzi wa kuanzisha utaratibu wa Kushughulikia, Kuzuia na kutanzua migogoro, Agenda ya Utekelezaji iliyoridhiwa Cairo, June 1995, ushindi dhidi ya Ukoloni na Ubaguzi wa rangi na hivyo kutoa fursa kwa kuchipua kwa dola mpya za Kidemokrasia Afrika ya Kusini na kuchipuka kwa mfumo wa siasa wa vyama vingi barani Afrika, vyote viliashiria dhamira mpya ya kulinasua bara letu kutoka katika hali ya dhiki na umaskini unaotokana na maendeleo duni. Dhamira hiyo iliambatana na kutambua ukweli kwamba maendeleo ya kweli ya

bara letu yatapatikana kwa kutegemea zaidi mchango wa nguvu na maarifa ya Waafrika wenyewe katika kila nchi na kwa Bara zima.

Kuchomoza na kushamiri kwa mkondo wa utandawazi, na kuongezeka kwa kasi ya mzunguko wa bidhaa na huduma na pia mabadiliko makubwa ya maendeleo ya Sayansi na teknolojia na hususan katika fani ya teknolojia ya mawasiliano na upashanaji habari vilileta matumaini mapya kwa Bara la Afrika. Hata hivyo maendeleo hayo katika mazingira ya Utandawazi yalizua hofu na vitisho vipya na athari mpya ambazo ni muhali kwa ustawi wa bara letu. Vyote vilihitaji nguvu za pamoja kuvikabili. Kunako mwisho wa karne ya 20 suala la ulazima wa mabadiliko lilikuwa haliepukiki.

**MPANGO WA KUFUFUA UCHUMI MIKAKATI YA KULETA MAENDELEO ENDELEVU: MAP, OMEGA HADI NAI**

Tukio moja kubwa la kihistoria litakaloendelea kukumbukwa kwa kipindi kurefu, ni lile lililotolea wakati wa Kikao cha 4 cha Dharura cha Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Nchi huru za Afrika uliofanyika mjini Sirte, Libya ambapo lilitolewa Tamko la Sirte tarehe 9 Septemba 1999. Tamko hilo

lilihusu uamuzi wa kutekeleza matarajio ya muda mrefu wa Waafrika na kuunda Umoja wa Bara la Afrika.

Ilikuwa katika kujadili matatizo na changamoto zinazolikabili bara letu katika mazingira ya dunia ya utandawazi ndipo Wakuu hao wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika walipowakabidhi Marais Thabo Mbeki wa Afrika Kusini, Olusegun Obasanjo wa Nigeria na Abdelaziz Buteuflika wa Algeria, jukumu la kutafiti ni jinsi gani Afrika inaweza kujikwamua kutoka mnyororo wa Madeni. Wakati wa kutekeleza jukumu hili walilokabidhiwa, Rais Thabo Mbeki alipata fikira mpya na kupendekeza mpango wenye upeo mpana zaidi ya ule ambao lengo lilikuwa ni kushughulikia suala la kujikwamua na mzigo wa madeni tu. Mpango huo unazingatia mafasi ya Afrika ndani ya mfumo wa mahusiano ya Kisiasa na Kiuchumi duniani na kupendekeza hatua muhimu ambazo hazina budi kuchukuliwa kukabili na kuikabili hali hiyo – na hivyo kuliweka bara letu katika njia sahihi itakayolielekeza bara hili katika maendeleo na usatwi. Mpango huu uliobuniwa na Rais Thabo Mbeki na kuafikiwa na wenzake uliitwa Ubia wa Millenia kwa Afrika (Millenium Partnership for Africa, MAP).

Wakati akina Thabo Mbeki na wenzake wakibuni mpango wa MAP, Rais Abdoulaye Wade wa Senegal naye alikuwa akilitafakari suala la hatma ya Bara la Afrika katika ulimwengu wa utandawazi na hatua zinazostahiki kuchukuliwa kuliwezesha kuhimili mikiki-mikiki na athari ziletwazo na nafasi na mchango wetu duni katika uchumi wa dunia. Tafakuri yake ilimuwezesha kubuni mpango aliouita OMEGA.

Kikao cha Tano cha Dharura cha Wakuu wa Nchi Huru za Afrika kilichofanyika Sirte, Libya March 2001 kiliridhia kuainisha maudhui na malengo ya MAP na yale yaliyomo katika OMEGA, kazi ambayo ilifanywa na Mawaziri wa Fedha na Maendeleo ya Uchumi katika kikao chao kilichofanyika Algiers, Algeria May, 2001. Matokeo ya kazi hii ni mpango ulioainishwa na kuhuishwa ambao ulikuja kujulikana na DHAMIRA MPYA YA AFRIKA, New African Initiative (NAI) uloridhiwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi Huru za Afrika katika kikao chao cha Lusaka 11 Julai, 2001. Kikao hicho pia kiliidhinisha kuundwa kwa Kamati ya Wakuuwa Nchi ya Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mpango huo.

Itakumbukwa kwamba wakati jitihada hizi zilikuwa zikifanywa chini ya uratibu wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika, jitihada nyingine zilikuwa zikipendekezwa kutoka sehemu na taasisi mbalimbali kwa madhumuni yale yale ya kulikwamua Bara la Afrika ili lijinasue kule lilikonasa hata kusababisha kuvia au hata kuporomoka kwa maendeleo kidogo yaliyoanza kupatikana katika miongo miwili au mitatu ya kwanza kufuatia miaka ya 1960. Kwa mfano sambamba na MAP na OMEGA, Tume ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa kwa Afrika (ECA) nayo ilibuni mkakati uliojulikana kama COMPACT for Africa. Mpango huo haukufika mbali kwa vile iliamuliwa kuwa nguvu zaidi zielekezwe kuhuisha na kuimarisha mipango ile miwili ya OMEGA na MAP. Ni muhimu kusisitiza kuwa NAI ilitokana na juhudi na tafakuri za Waafrika, ni mpango uliobuniwa na Waafrika kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi endelevu wa matatizo na changamoto mbalimbali zinazolikabili Bara la Afrika.

Lakini kwa kuzingatia uzito wa matatizo na changamoto hizo, kwa kutambua kuwa uwezo ndani ya Bara lenyewe peke yake havitoshelezi kupata ufumbuzi wa kukidhi haja na vile vile kwa kutambua ukweli kwamba Bara la Afrika limekuwa mshiriki katika

kuchangia maendeleo ya ulimwengu kwa jumla na hivyo linayo haki kudai jumuiya ya Kimataifa kushiriki katika kuchangia maendeleo ya bara hili, jina la mpango lilibadilishwa kutoka "NEW AFRICAN INITIATIVE (NAI)" na kuwa "NEW PARTNERSHIP FOR AFRICAN DEVELOPMENT (NEPAD)" mwezi Oktoba 2001 na hivyo kusisitiza umuhimu wa kushirikisha wadau wote ndani ya nchi, baina ya nchi katika Afrika na baina ya Afrika na Washirika wake ulimwenguni.

Imetupasa kurejea chimbuko la NEPAD ili kusisitiza kuwa huu ni mpango asilia wa Waafrika ambao chimbuko lake ni kutokana na hali halisi ya uduni wa maisha yetu na kupuzwa au kutokuwa na kauli hata katika masuala muhimu yanayogusa maisha yetu. Aidha ni mpango unaotokana na uzoefu tulioupata katika kutekeleza mipango ya pamoja katika bara letu na kutiwa matumaini na hazina ya raslimali zilizomo katika bara hili na changamoto zinazotukabili katika Millenia hii mpya.

**NEPAD NI MPANGO WA AFRIKA KWA AJILI YA UKOMBOZI WA AFRIKA**

NEPAD ni matokeo ya uamuzi wa pamoja toka kuasisiwa kwake hadi uliporidhiwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi Huru za

Afrika na kuanisha na kukasimu majukumu katika kila hatua. Kwa hali hiyo, katika hali ambapo chimbuko lake linatokana na vuguvugu lile lile na matarajio ya viongozi wale wale walioasisi taasisi zilizozaa Umoja wa Afrika, haitarajiwi basi kuwepo mgongano katika malengo na madhumuni ya Umoja wa Afrika na yale ya NEPAD, kama ambavyo wale wasiotutakia mema wamekuwa wakiashiria. Tangu mwanzo NEPAD ililenga kutekeleza madhumuni ya Umoja wa Afrika. NEPAD inasimama katika nguzo imara ya mahusiano ya kutegemeana kati ya mpango wa Umoja wa Afrika na si mpango mbadala nje ya huo wa Umoja wa Afrika.

Kimaudhui, NEPAD ni mkakati wa bara hili wenye lengo la kuleta uamsho mpya wa maendeleo ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi. Ni mpango wenye dhamira ya kuimarisha misingi ya utawala bora kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo, kuhimili amani na utengemano na kuandaa mazingira adhimu kuliwezesha bara hili kushiriki kikamilifu katika shughuli mbali mbali katika jamii ya Kimataifa.

**MALENGO YA NEPAD**

Malengo makuu ya NEPAD ni haya yafuatayo:

- Kuondosha umaskini uliokithiri;
- Kuchochea kasi ya kukua kwa uchumi na maendeleo endelevu;
- Komesha mwelekeo wa bara letu kuweko pembezoni katika mkondo wa kushamiri kwa utandawazi;
- Kurejesha amani, usalama na utulivu na utengemano katika bara.

**MSISITIZO NA KIPAUMBELE**

Mkazo katika mkakati wa NEPAD umewekwa katika yafuatayo>

(a) Kurejesha hali ya amani, usalama na utulivu

(b) Kujenga misingi na kanuni za utawala bora

(c) Kufufua kazi ya kukua kwa uchumi na maendeleo endelevu

(d) Kupunguza umaskini na tofauti ya mapato katika jamii

(e) Kuimarisha mafanikio kujenga demokrasia na kuimarisha taasisi na asasi za kidemokrasia

(f) Kukarabati miundo-mbinu iliyochakaa na kujenga miundo-mbinu ya kiuchumi mipya pale panapohitajika

(g) Kutafakari upya misingi na aina ya ushurikiano wetu na wadau wengine na kushiriki kikamilifu katika kufanya mabadiliko katika sera na miundo na taratibu za uendeshaji

wa Taasisi na asasi za fedha zinazohimili mfumo wa uchumi wa dunia.

(h) Kupunguza pengo katika matumizi ya teknolojia ya Kisasa na mawasilano na upashanaji habari.

Mkazo katika mkakati mzima wa NEPAD umewekwa katika kujenga aina mpya ya mahusiano na ushirikiano baina ya wadau mbalimbali kuanzia ndani ya nchi husika, baina ya nchi za Kiafrika zenyewe na baina ya nchi hizo na Washirika wengine duniani. Kwa mantiki hiyo NEPAD inaweka mkazo mkubwa kwenye suala la ushirikishwaji wa umma katika kila nchi kupitia taratibu muafaka za ubia baina ya asasi za dola, sekta binafsi na jumuiya huru za kijamii. Katika ngazi ya bara zima msisitizo ni kwenye ushurikiano katika kujenga na kukuza uwezo, kukusanya nguvu na raslimali na katika kukabiliana na kutanzua changamoto zilizopo na zitakazojitokeza. Katika ngazi ya ulimwengu, inatarajiwa aina mpya ya ushirikiano baina ya Afrika na Washirika wetu utachipua hatua kwa hatua. Msingi mkubwa wa ushirikiano huo mpya unatarajiwa kujengeka kwa kuzingatia maslahi muafaka ya pande husika lakini huku ukiruhusu ongezeko la mitaji na uwekezaji kwa lengo la

kusaidia kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi wa Afrika na vile vile kufungua milango ya masoko katika nchi zilizoendelea kwa bidhaa za Afrika.

## MAHITAJI NI MAKUBWA KULIKO UWEZO

Mpango wa NEPAD, kama tulivyoeleza hapo juu ni mpango wa Waafrika kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya Afrika. Kwa hiyo suala la umiliki na jukumu usimamizi wa utekelezaji wa mpango wenyewe ni la Waafrika wenyewe. Mafanikio au kutofanikiwa kwa mpango huu kutategemea ni kwa kiasi gani Afrika itategemea ni kwa kiwango gani rasilimali za bara hili na ubunifu na uadilifu wa watu wetu vinatumika kwa ukamilifu. Hata hivyo tunatambua unyonge wetu na ukomo wa uwezo tulionao uilinganisha na uzito wa changamoto zinazolikabili bara letu. Tunatambua kuwa ili kujenga uwezo wa kukabili matatizo makubwa yanayotukabili kwa pamoja kama bara, kupunguza kiwango cha umasikini uliokithiri ambao ni moja ya vikwazo vikubwa kwa maendeleo, Uchumi wa Afrika sharti ukue kwa kiwango cha asilimia saba (7%) kwa mwaka. Kiwango hiki cha kukua kwa uchumi kinahitaji kiwango cha uwekezaji cha

asilimia kati ya 10% hadi 15% ya Pato la Ndani la Jumla (GDP) la Bara la Afrika.

Viwango hivi vya ukuaji na uwekezaji vikitafsiriwa katika fedha, imekadiriwa Afrika itahitaji raslimali za ziada takriban Dola za Kimarekani billioni 64 kwa mwaka ili kufikia malengo yaliyowekwa katika mpango wa NEPAD. Matarajio ni kwamba kiwango hicho kinaweza kupatikana kwa njia zifuatazo:

- Ongezeko katika kukuza Akiba ya ndani na kuimarisha vyanzo na taratibu za ukusanyaji wa mapato ya Serikali
- Ongezeko la mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa katika masoko ya nje na uwekezaji
- Mitaji toka wawekezaji wa nje
- Misamaha ya madeni kwa nchi za Kiafrika
- Misaada ya maendeleo.

**KUZINGATIA UTAWALA BORA NA DHANA YA KUKOSOANA KINDUGU**

Jambo moja kubwa lililobuniwa kama sehemu muhimu ya Mpango wa NEPAD ni utaratibu wa kuhakikiana kwa viongozi wetu (Peer Review Mechanism). Utaratibu huu unatokana na uamuzi uliofanywa katika Kikao cha Kwanza cha Kamati ya

usimamizi wa utekelezaji wa Mpango wa NEPAD. Iliazimiwa katika kikao hicho kwamba:

> "…. Imekubalika kwamba viongozi wa Afrika wajiwekee vigezo vya Utawala Bora ili view mwongozo katika kutekeleza majukumu ya ya Kisiasa na Kiuchumi. Kwa hali hiyo, imeamriwa kwamba katika kikao kijacho Kamati itapokea, kutafakari na kuridhia utaratibu muafaka wa kuhakikiana (kupimana) wenyewe kwa wenyewe pamoja na maadili yanayoendana na utaratibu huo…"

Utaratibu huo wa kuwekana sawa uliandaliwa mapema mwaka 2002 pamoja na Tamko rasmi juu ya "Demokrasia, Uongozi wa Kisiasa, Kiuchumi na Kijamii na yote mawili yaliwasilishwa katika Kikao cha Wakuu wa Umoja wa Afrika katika kikao chao cha Durban, Afrika Kusini Julai 2002. Madhumuni ya utaratibu huu wa kuhakikiana (kupimana) wenyewe kwa wenyewe (APRM) ni pamoja na yafuatayo:-

> "Kuwezesha kuendeleza sera, vigezo, maamuzi na vitendo vinavyolenga kuimarisha hali ya utulivu na amani, viwango vya juu vya ukuaji wa uchumi, maendeleo endelevu na kasi

zaidi ya ushirikiano kikanda na bara zima kwa kubadilishana uzoefu na mbinu ziliofanikisha utekelezaji wa mambo ambazo ni mfano wa kuigwa na wengine na vilevile kubaini mapungufu na mahitaji katika kujenga uwezo."

Kwa hakika utaratibu huu unalenga kuziwajibisha dola zote za Kiafrika kujihusisha kuelewa kile kinachoendelea katika nchini nyingine za Kiafrika na pale ambapo hapana budi kuwajibika kwa pamoja kutafuta ufumbuzi wa tatizo, kuondoa kasoro au kusaidia kuongeza uwezo penye upungufu. Tumeonewa vya kutosha kama bara, tumepuuzwa vya kutosha kama bara, ili tusionewe wala kupuuzwa tena lazima tuwajibike kwa pamoja. Huu ndio ujumbe mkuu na mantiki ya Utaratibu huu wa kuwekana sawa. Katika utaratibu huu, dola itaitathimini dola nyingine. Aidha ndani ya utaratibu huu zimeundwa asasi mahsusi kwa kufanya kazi hiyo. Hatimaye lengo ni kusaidia dola ile iliyogundulika kuwa na mapungufu kufanya marekebisho katika sera zake na taratibu za kiutendaji kwa kujifunza kutoka mafanikio yaliyodhihirika mahali pengine na kwa hiyo basi kuisaidia nchi husika kuzingatia maadili, vigezo na misingi iliyowekwa.

**KIPYA NI NINI KATIKA NEPAD?**

Tunaweza kujiuliza ni kwa kiasi gani basi NEPAD inatofautiana na jitihada nyingine zilizotangulia zikiwa na malengo kama haya kwa mfano Mkataba wa Abuja wa 1991 ambao lengo lake ilikuwa kuanzisha Jumuiya ya Uchumi ya Bara la Afrika, au Agenda ya Cairo ya 1995 kuhusu Agenda ya Maendeleo ya uchumi na Kijamii ya Bara la Afrika. Jibu ni kwamba NEPAD hatofautiani na jitihada na maamuzi hayo yaliyotangulia kwa maana kwamba zote ni jitihada zinazolenga kujenga Afrika yenye uwezo na kauli katika Ulimwengu wa leo. Lakini NEPAD imejengeka katika msingi wa uzoefu tulioupata wakati tukiyatekeleza maamuzi na mipango ya awali. Si vibaya tukakiri kwamba mafanikio yanayotokana na utekelezaji wa mipango iliyotokana na maamuzi hayo ni nadra sana.

NEPAD inakiri kuwepo kwa mfungamano tegemezi baina ya azima ya Kisiasa na matakwa halisi ya Kiuchumi na Kijamii. Wakati umuhimu wa utawala na uongozi bora wa Kisiasa na Kiuchumi imezingatiwa, NEPAD imejielekeza zaidi kwenye mipango ya kimkakati na umuhimu wa kuunda mazingira adhimu ya uhusiano wa Kimataifa yatakayolinufaisha Bara la Afrika katika

jitihada za kujikwamua kimaendeleo. Isitoshe NEPAD inasisitiza kuimarisha mahusiano ya kiubia baina ya sekta ya dola, sekta binafsi na Jumuiya za Kijamii. Kwa ujumla NEPAD inaelekeza juhudi zaidi kwenye kufanikisha matarajio ya bara hili bila kuyafumbia macho au kuyapuuza mazingira halisi ya karne hii ya 21.

Kuna baadhi wameonyesha wasiwasi kwamba kufanikiwa au kutofanikiwa kwa NEPAD kutategemea ni kwa kiasi gani Afrika itafanikiwa kuvutia mtiririko wa raslimali za ziada kwa kiasi cha Dola za Kimarekani billioni 64 kwa kila mwaka kuwezesha Uchumi kukua kwa asilimia saba (7%). Hakika pamoja na matamko ya kupongeza jitihada hii na kauli za kuunga mkono NEPAD zilizotolewa na nchi za Magharibi, ukweli hadi sasa unaonyesha kwamba kauli hizo hazikuambatana na dhamira za kweli za kutenga raslimali za kutosha kukidhi mahitaji ya kutekekeza mpango huo kw aufanisi na kwa kiwango cha kuridhisha. Hali hii haitii moyo iwe ni katika kutoa upendeleo maalum kufungulia bidhaa za Afrika kuingia katika masoko ya nchi zilizoendelea au kuongeza viwango vya misaada ya maendeleo. Bado kuna kazi za kufanya katika eneo hili, na tusitarajie miujiza.

## UHUSIANO WA NEPAD NA UMOJA WA AFRIKA

Suala jingine ambalo linaweza kuulizwa ni uhusiano baina ya Umoja wa Afrika na NEPAD. Ni muhimu kufafanua uhusiano huu kwa sababu baadhi ya wale wasiolitakia mema bara hili wamejitahidi kujenga hisia kwamba NEPAD ilibuniwa maksudi kudhoofisha jitihada za kuimarisha AU na hivyo kujenga Umoja wa Afrika. Hisia hizi zinaimarishwa na kiwango kidogo ambacho nchi za magharibi zimeunga mkono au angalau kushabikia uamuzi wa kuunda AU badala ya OAU kama ambavyo wameonyesha kushabikia mpango wa NEPAD.

Ninarejea kusisitiza kuwa hakuna mgongano baina ya malengo ya AU na yale ya NEPAD. Ukweli huo umedhihirishwa na kauli ya hivi karibuni ya Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji kwamba NEPAD ni programu ya Umoja wa Afrika. Ndio mwongozo wa AU kutekeleza madhumuni yake na utaratibu wa kuongeza kasi ya kutekeleza Mkataba wa Abuja wa 1991. Kwa hakika, uchunguzi wa Programu za NEPAD na maeneo yaliyopewa umbele katika mpango huo ikifanywa kwa makini na bila hila wala huba, utadhihirisha kwamba hakuna mahali popote ambapo programu za

NEPAD zinakinzana au kwenda kinyume na malengo ya Umoja wa Afrika.

Isitoshe, kamati ya utekelezaji ya NEPAD inatoa taarifa zake kila mwaka kwa Wakuu wa Umoja wa Afrika. Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika wakati wa kipindi cha Uenyekiti wake ni Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa NEPAD. Kamisheni ya Umoja wa Afrika, hushiriki katika vikao vya Kamati Maalum ya NEPAD katika kikao chao cha hivi karibuni Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji waliagiza ifuatavyo:

> *"Uhusiano baina ya Umoja wa Afrika na Sekretariati ya NEPAD kuanzia sasa ujidhihirishe kwa kuwapo kwa ushirikiano wa karibu katika kuandaa mipango ya utekelezaji na kuiratibu Sekretarieti ya NEPAD ichukuliwe kuwa ni asisi ya mpito yenye lengo la kuhudumia Kamati ya Wakuu wa Nchi ya Utekelezaji wakati tukisubiri kukamilisha kuundwa kwa taasisi ya kudumu za Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Wakati utafika ambapo NEPAD itakuwa ni moja ya taasisi au asasi za kudumu katika muundo wa Umoja wa Afrika".*

**NINI WAJIBU WETU NA MATARAJIO**

Mwisho, kwa jinsi gani nchi kama yetu ijihusishe na mpango wa NEPAD na kwa matarajio gani?

Kama nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika na kwa hakika mwanachama hai makini na mshiriki wa kutegemewa, Tanzania inajishughulisha na Mpango wa NEPAD katika medani mbili – kwanza ni kwa kutekeleza majukumu yake kama mwanachama mwingine yoyote wa Taasisi, Uhusiano wa Kitaasisi. Pili ni katika kubuni na kutekeleza mipango na programu za NEPAD na kuziainisha na kuzijumuisha katika mipango ya taifa. Dhamira ya msingi ya NEPAD ya kukuza mfungamano kati ya utawala bora, maendeleo na ushirikiano baina ya mataifa unarandana na falsafa ya maendeleo ya Tanzania. Isitoshe kwa kuwa NEPAD intoa fursa ya kushughulikia changamoto za maendeleo zinazotukabili kwa pamoja kama bara, dhamira hii inachangia kuimarisha matarajio ya muda mrefu ya Watanzania kuona ushirikiano zaidi baina ya nchi za Kiafrika hatimaye kufikia Umoja wa Afrika.

Na zaidi ya hayo, na pengine la msingi zaidi ni kwamba utekelezaji wa Progaramu za NEPAD na miradi ya Kisekta iliyopewa

kipaumbele hufanyika haswa katika ngazi ya Kanda au Kitaifa. Kwa hiyo, Tanzania haina budi kushiriki katika kubuni na kuandaa mipango na miradi mbalimbali kwa kushirikiana na nchi wanachama wenzao katika kanda husika ili kujihakikishia kuwa maslahi ya Kitaifa yamezingatiwa na tunanufaika na utekelezaji wa mipango na programu hizo. Utekelezaji wa miradi kama ujenzi wa miundo-mbinu ya Kiuchumi, ukuzaji wa uwezo kupitia mafunzo na maendeleo ya nguvukazi, kilimo, hifadhi na matumizi endelevu ya mazingira, utamaduni na ukuzaji wa Sayansi na teknolojia ni baadhi ya mifano michache ambayo inaweza kutunufaisha kama taifa kwa kushiriki kikamilifu katika Programu za NEPAD.

Lakini, hatimaye manufaa yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa programu za NEPAD kwa nchi kama Tanzania kwanza sharti yatazamwe katika mustakabali wa bara zima na manufaa ya ziada yatakayotokana kuwepo mahusiano mapya na mfumo usio na vikwazo kwa maendeleo yetu; mfumo ambao unatuwekea mazingira adhimu yanayotuwezesha kutumia raslimali zetu na kukuza vipaji vyetu kwa ukamilifu na kunufaika na faida zitokanazo na aina mpya ya ushurikiano wa kiuchumi kwa misingi ya haki kwa washiriki wa pande husika.

Zaidi ya yote, kwa kuweka msisitzo katika kujenga mfungamano baina ya utawala bora, maendeleo na ustawi wa watu uliojengeka katika mahusiano ya ushirikiano na mshikamano, Tanzania ambayo wakati wote tangu kupata uhuru wake imesifika kwa kuweka mbele maendeleo ya watu kuliko kitu kingine inayo mengi ya kutarajia kutokana na kushiriki kwake katika utekelezaji wa NEPAD.

**INAWEZEKANA, TUWAJIBIKE**

Hakika, ndoto ya muda mrefu ya Mwafrika ni matarajio ya kuliona bara lenye uwezo mkubwa wa Kiuchumi na Kisiasa, uwezo unatokana na mshikamano wa dhati, bara lililo na amani na utulivu, bara linatotekeleza wajibu wake na kuchukua nafasi stahiki katika jumuiya ya Kimataifa na bara ambao watu wake wamefanikiwa kuondoa unyonge utokanao na umaskini uliokithiri, maradhi na ujinga. Hii ni ndogo njema inayoweza kugeuzwa kuwa ukweli kupitia utekelezaji kwa dhati tukitumia juhudi na maarifa mipango na programu ya NEPAD.

Na linawezekana.